HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA RUKWA MHE. DANIEL OLE NJOOLAY KATIKA UWANJA WA NELSON MANDELA MJINI SUMBAWANGA WAKATI WA UZINDUZI WA SIKU YA SHEREHE ZA SIKU YA SERIKALI ZA MITAA MWAKA 2011, TAREHE 24 JUNI, 2011

Mheshimiwa Mwenyekiti wa ALAT Taifa Diwani Masaburi,
Waheshimiwa Wabunge,
Waheshimiwa Wenyeviti wa Halmashauri mlioko hapa Rukwa,
Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,
Waheshimiwa Viongozi wa Madhehebu mbalimbali ya Dini,
Viongozi na Watumishi wa Umma,
Wageni waalikwa,
Mabibi na Mabwana.

Awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru waandaaji wa Sherehe hizi za Siku ya Serikali za Mitaa kwa kunialika kufungua rasmi sherehe hizi.

Napenda vile vile kuwashukuru kwa mipango na maandalizi mazuri ambayo nimeweza kuyaona hapa kwenye viwanja hivi vya Nelson Mandela.
Hongereni sana.

Nawashukuruni pia washiriki wote katika mabanda yote yanayozunguka uwanja huu ambao wameweza kuleta vifaa, nyenzo na maelezo yanayohusu shughuli wanazozitekeleza katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Ndugu Wananchi,

Kauli mbiu ya sherehe za mwaka huu **SHEREHEKEA MIAKA 50 YA UHURU KWA KUIMARISHA UGATUAJI WA MADARAKA KWA WANANCHI KWA MAENDELEO YAO** inasisitiza maudhui na madhumuni hayo. Madhumuni ya kuundwa kwa Serikali za Mitaa katika nchi yetu ni:-

(a) Kuwa na vyombo vinavyotokana na Wananchi wenyewe na vinavyofanya **kazi *ya kuinua ustawi na uchumi wa Wananchi***.

(b) Kuhakikisha ***kunakuwepo kwa Ulinzi na Usalama wa Wananchi*** na mali zao.

(c) Kuhakikisha kuwa ***wananchi wanapatiwa huduma za jamii wanazohitaji kwa njia isiyo wapatia bughugha au malalamiko***.

(d) ***Kuunga mkono kila inapowezekana juhudi za wananchi*** wanazozianzisha zinazolenga katika kujiletea Maendeleo yao wenyewe.

(e) ***Kuwajengea Wananchi mazingira yatakayowawezesha kuongeza*** kasi ya kujiletea maendeleo.

Wakati huu tunapoadhimisha miaka 50 ya Uhuru ni muhimu mamlaka za Serikali za Mitaa zichukue hatua kuondoa mapungufu na kasoro zilizokuwa zimedhihirika katika utendaji wake. Kasoro hizo ni pamoja na:

a) Halmashauri kutojibu hoja za ukaguzi kama linavyotakiwa;

b) Halmashauri kushindwa kuweka vivutio ili kuwezesha utekelezaji wa **KILIMO KWANZA** kama vile kuboresha miundombinu ya umwagiliaji;

c) Halmashauri kushindwa kuwa na mipango ya mafunzo kwa Watumishi na kuingiza kwenye bajeti ili kuondoa manunguniko hususan katika Sekta ya Elimu;
d) Halmashauri kushindwa kusimamia misingi na Kanuni za utawala bora ikiwa ni pamoja kuondoa mianya ya rushwa;
e) Halmashauri kushindwa kuona umuhimu wa kuwavutia kwa makusudi wawekezaji katika maeneo yao.
f) Aidha, ni muhimu sana Halmashauri zishirikishe kikamilifu wananchi kwa mfumo wa O & OD katika kuibua miradi yao mbalimbali (si suala la wataalamu peke yao).

Katika Mkoa huu wa Rukwa, ambako sherehe hizi zinafanyika Kitaifa, Halmashauri zote zimejiandaa ipasavyo kusherehekea siku hii katika maeneo yao, kama ilivyo kwa maeneo mengine nchini. Miradi mbalimbali itazinduliwa wakati wa wiki hii ya Serikali za Mitaa inayofikia kilele Ijumaa tarehe 01 Julai 2011

Ndugu wananchi,
Suala la kuimarisha Serikali za Mitaa ili ziweze kuwa vyombo madhubuti vya kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo ya kijamii ya wananchi kwenye maeneo yao, halina mjadala. Wananchi washirikishwe ipasavyo katika kupiga vita umaskini katika maeneo yao.

Ndugu Wananchi,
Maadhimisho haya ya siku ya Serikali za Mitaa yanaenda sambamba na maadhimisho ya miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara. Kauli mbiu yake kitaifa "**TUMETHUBUTU, TUMEWEZA, TUNAZIDI KUSONGA MBELE**". Maadhimisho haya yanatuweka katika nafasi ya kujitathmini tulipotoka, tulipo sasa na

tunapokwenda. Ni wazi kuwa nchi ilipotoka sio ilipo hivi sasa, yapo mengi ambayo yamefanywa na Serikali ambayo ni ya kujivunia; mfano: Katika kipindi hicho, mengi sana yamefanyika Mkoani kwetu, kama ifuatavyo:-

KILIMO
- Tunazalisha mara sita ya mahitaji yetu.
- Ni Mkoa wa kwanza kwa matumizi makubwa ya plau (70% ya kilimo ni plau).

ELIMU
- Tulikuwa hatuna shule hata moja ya Sekondari. Sasa tunazo
- shule 115 za serikali na Binafsi
- Tulikuwa na shule 10 tu za Msingi, sasa ni 504
- Tulikuwa hatuna chuo chochote. Sasa tuna vyuo vitatu vya Elimu, Vyuo vya Afya viwili, Chuo cha VETA n.k.

AFYA:
- Tulikuwa hatuna hospitali hata moja. Sasa tunazo 4, na vituo vya afya 34 na Zahanati nyingi.

MIUNDOMBINU:
- Tulikuwa tunapitia Zambia, ili kuzungukia Tunduma. Tuende
- Dar es Salaam. Sasa barabara ya Tunduma – Sumbawanga
- inajengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, Mkoa sasa unaendeka
- kwa barabara karibu kila kona.

VIWANDA:
- Tulikuwa hatuna hata kiwanda kimoja. Mkoa wetu ulikuwa
- 'labour reserve' sasa tunavyo viwanda kadhaa vya usindikaji
- vyakula, na viwanda vingi vidogo-vidogo.

Kwa sasa hatua tuliyopiga ni nzuri na ya kujivunia, cha muhimu ni kushikamana, kuacha tofauti zetu, kufanya kazi kwa bidii na kuweka maslahi ya nchi mbele.

Ndugu Wananchi,

Napenda kuwahimiza viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Mkoa huu wawasaidie wakulima kwa kuwapatia huduma stahili za ugani ili wazalishe chakula cha kutosha na hivyo kujikwamua na umasikini.

Mwisho ninapenda kumalizia mazungumzo yangu nanyi kwa kuwashukuru kwa mara nyingine waandaji wa sherehe hizi na kuwaomba muendelee kutambua kwamba Serikali za Mitaa ni vyombo vyenu na hamna budi kuvitumia ili kupata maendeleo na kutatua kero zenu.

Kwa kuwa sherehe hizi zinafunguliwa rasmi leo, ninachukua nafasi hii kuwaomba kuwa muendelee kushiriki kwenye maonesho yanayoendelea na kuwahimiza kujitokeza kwa wingi siku ya kilele cha sherehe hizi hapo tarehe 1 Julai, 2011.

Ninapenda kutamka kwamba Sherehe za Siku ya Serikali za Mitaa kwa mwaka 2011 zimefunguliwa rasmi.

Ahsanteni kwa Kunisikiliza

Daniel Ole Njoolay
MKUU WA MKOA
RUKWA